

**MKATABA WA PANGO
KATI YA**

MASELE MISUNGWI

NA

DF METAL MINING LIMITED

**UPANGAJI WA SHAMBA LILILOPO KATIKA KIJIKI CHA IKUNGUMHULU, KATA
YA IKUNGUMHULU, WILAYA YA MISUNGWI MKOA WA MWANZA.**

**MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI.
MAKUBALIANO YAMEFANYIKA LEO TAREHE 01/10/2024**

KATI YA

MASELE MISUNGWI (Ambaye kwa mujibu wa makubaliano haya atajulikana kama (“Mmiliki”) kwa upande mmoja;

NA

DF METAL MINING LIMITED S.L.P 79987, DAR ES SALAAM. (Ambaye kwa mujibu wa makubaliano haya atajulikana kama (“Mpangishaji”) kwa upande mwingine;

HIVYO MAKUBALIANO HAYA YANASHUHUDIA KWAMBA:

1. Miliki anamkodisha Mpangishwaji Ardhi husika kutoka kwa Mmiliki kwa kiasi cha Shilingi Million Mbili na laki tano (2,500,000/=) kwa kila baada ya Mwaka Moja ambayo kila baada ya miaka 2 ni Tshs Milioni Tano (Tshs.5,000,000) tu, kwa kipindi cha Miaka kumi (10) tokea siku ya kuanza kwa Mkataba huu yaani kuanzia tarehe 01/10/2024
2. Ardhi inayokodishwa ni shamba lililopo kwenye kijiji cha Ikungumhulu, Kata ya Shilalo, Wilaya ya Misungwi mkoa wa Mwanza
3. Mmiliki amemkabidhi Mpangishaji Ardhi hiyo mara baada ya kusainiana Mkataba huu, na ambapo Nyaraka zote zinazohusu manunuzi na umiliki wa Ardhi hiyo zimebaki kwa Mmiliki.
4. Kwamba, Mkataba huu hautoweza kupangishwa kwa mtu mwingine.
5. Mmiliki wa Ardhi endapo akihitaji kuvunja mkataba atahitaji kumlipa Mpangishaji DF METAL MINING LIMITED kiasi cha USD \$10,000,000.
6. Ndani ya muda wa miaka 10 kodi ya Ardhi haita badilika kulingana na makubaliano ya Mkataba.
7. Katika kipindi cha mkataba wa miaka 10 hauwezi kurejesha haki ya matumizi ya ardhi.
8. Makubaliano haya yamefanyika chini ya Uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Ikungumhulu, Kata ya Shilalo, Wilaya ya Misungwi, Jiji la Mwanza na endapo kutatokea kutoelewana basi upande wowote unayo haki ya kufuata taratibu za kisheria.

Makubaliano haya yamefanyika leo na kutiwa sahihi na pande zote mbili kama inavyoonekana hapa chini:-

JINA LA MMILIKI: MASELE MISUNGWI

SAHIHI: M. N. NGURILA

TARAHE: 01-10-2024

MASELE MISUNGWI



JINA LA MPANGISHWAJI: DF METAL MINING

LIMITED SAHIHI 李 小 卫

XIAOWEI LI- Mkurugenzi

TAREHE 01-10-2024

JINA LA SHAHIDI WA MPANGISHAJI Viktor Mgweno

SAHIHI V Mgweno

TAREHE 01-10-2024

